

AHMED ESSA NA OTHMAN ALI



KUUFHAMU USTAARABU *wa* KIISLAMU

Mchango wa **WAIISLAMU** *katika*
MWAMKO NA MAENDELEO

■ SWAHILI VERSION

Idara ya Lugha na Ukalimani ya Chuo Kikuu
cha Waislamu cha Morogoro

IIIT — Mfululizo wa Vitabu kwa Muhtasari

**KUUFHAMU
USTAARABU
wa KIISLAMU**

Mchango wa **WAISLAMU** *katika*

MWAMKO NA MAENDELEO

■ **SWAHILI VERSION**

Idara ya Lugha na Ukalimani ya Chuo Kikuu
cha Waislamu cha Morogoro

©International Institute of Islamic Thought, 2012

International Institute of Islamic Thought (IIIT)

P.O.Box 669

Herndon, VA 20172, USA

www.iiit.org

16 / 03/ 1429 AH 24/ 03/ 2008 AD

ii
Hakimiliki ya Kitabu hiki imehifadhiwa. Hairuhusiwi kukipiga chapa, kwa namna yoyote ile bila ruhusa ya maandishi ya wachapaji.

Rai na maoni yaliyo elezwa katika kitabu hiki ni ya mwandishi, na si lazima yatangamane na yale ya wachapaji.

Kimetafsiriwa na:

Abdallah Y. Tego

Kimehaririwa na:

Hadija Kutwa Abdallah

Design and layout by:

Iddi Suleiman Kikong'ona (iddkiko@gmail.com)

MFULULIZO WA MUHTASARI WA VITABU VYA IIIT



Mfululizo wa muhtasari wa Vitabu vya IIIT* ni hazina muhimu sana katika machapisho ya taasisi hii vilivyoandikwa kwa ufupi kabisa ili kumwezesha msomaji kuelewa dhamira kuu ya kitabu asilia. Vitabu vimeandikwa kwa ufupi ili kusomeka kwa urahisi na kuokoa muda hasa kwa waliotingwa na kazi. Machapisho haya yanatoa mwongozo wa dhima kuu, hivyo kumfanya msomaji kuwa na ari ya kutafuta nakala ya kitabu chenyewe.

Kuufahamu Ustaarabu wa Kiislamu, ni kitabu kilichotoka kwa ukamilifu mwaka 2010 na kutolewa mara ya pili mwaka 2011. Kitabu hiki kimetafiti maandiko ya Wasomi wa Magharibi ili kubainisha kuwa bila ya kuwepo mchango mkubwa wa kitaaluma kutoka Ulimwengu wa Kiislamu, hakika pasingelikuwepo Mwamko wa Maendeleo uliojiri Ulaya. Kwa takribani miaka elfu, Uislamu ulikuwa ndio ustaraabu unaoongoza duniani, ukivuka mipaka ya kijiografia na kushamiri, bila ya ubishi, kuliko ustaarabu wowote ule uliokuwepo. Uislamu uliondoa ubaguzi na utengano wa kijamii baina ya watu wa matabaka, kabila na utaifa, na ukaweka wazi kuwa watu wote wanastahiki kufaidi neema za dunia maadam hawakiuki taratibu na maadili. Uislamu ndio ulioanzisha taaluma ambazo, vinginevyo zingelipotea ama kwa karne nyingi, au moja kwa moja.

*. Ni ufupisho wa *International Institute of Islamic Thought* iliyo tafsiriwa kwa Kiswahili kama Taasisi ya Kimataifa ya Fikra ya Kiislamu

Uhodari na ubunifu wa Wanazuoni wa Kiislamu uliamsha na kuchochea utamaduni wa kisomi Ulaya na kwa takribani miaka mia saba lugha yake ya Kiarabu ilikuwa ndiyo lugha ya kimataifa iliyotumiwa rasmi katika sayansi. Kinacho shangaza sasa ni hii hali ya kupuuzwa urithi huu kwa makusudi, na wakati mwingine huzikwa kabisa. Kwa maneno ya Aldous Huxley, “Ukweli una nguvu, lakini bado kuna nguvu kubwa, kwenye mtazamo wa kutenda, ni kutousema ukweli. Kwa kutoyataja masuala fulani... wapakazaji wamefanikiwa kubadili uoni wa watu kwa upeo mkubwa kuliko mafanikio ambayo wangeyapata kwa kutumia ufasaha wa kuukanusha ukweli”.

Kwa hiyo, maudhui ya kuudhihirisha Ustaarabu wa Kiislamu ni hatua inayohitajika kuondoa upotoshaji huo na kurejesha upya ukweli wa kihistoria wa ‘zama za dhahabu’, au zama za nuru zilizo stawi katika mwamko wa maendeleo ya kiislamu, na ambayo ni matunda mengine ya Magharibi. Kwa kufanya hivyo, inapatikana fursa ya kuona upeo mpana wa mafanikio ya maendeleo ya utamaduni ambao umekubalika kuwa mfano bora wa ustawi na maendeleo ya mwanadamu katika kilele chake.

Toleo la Muhtasari la kitabu asilia walichoandika **Ahmed Essa na Othman Ali**, kwa lugha ya Kiingereza, kilichochapwa kwa jina la:

STUDIES IN ISLAMIC CIVILIZATION

The Muslim Contribution to the Renaissance

Ahmed Essa with Othman Ali

ISBN hbk: 978-1-56564-351-2

ISBN pbk: 978-1-56564-350-5

2012

Yaliyomo



NENO LA AWALI

v

UTANGULIZI

1

SURA YA KWANZA

Nafasi ya Uislamu Katika Historia *3*

SURA YA PILI

Elimu na Ustaarabu wa Kiislamu *5*

SURA YA TATU

Kuanzishwa Jamii ya Kwanza ya Kiislamu *7*

SURA YA NNE

Ulimwengu wa Kiislamu *9*

SURA YA TANO

Ustaarabu wa Kiislam Ulaya na Asia *11*

YALIYOMO

SURA YA SITA

Biashara 13

SURA YA SABA

Kilimo na Teknolojia 16

SURA YA NANE

Ustawi wa Elimu ya Uislamu 18

SURA YA TISA

Sayansi 21

SURA YA KUMI

Tiba 23

SURA YA KUMI NA MOJA

Fasihi ya Kiarabu 25

SURA YA KUMI NA MBILI

Fasihi ya Kiajemi 27

YALIYOMO

SURA YA KUMI NA TATU

Sanaa 29

SURA YA KUMI NA NNE

Mchango wa Dola ya Ottoman 31

SURA YA KUMI NA TANO

Mwamko Wa Maendeleo Ulaya 33

UTANGULIZI



Ustaarabu wa Kiislamu umeleta mafanikio makubwa na kuacha urithi wa kipekee ambao umeabadili ulimwengu, ukiwa umeenea sehemu kubwa duniani kuanzia Hispania na Afrika Kaskazini hadi Mashariki ya Kati na Asia, Uislamu ndiyo uliokuwa chimbuko la mwamko wa maendeleo Ulaya na dunia kwa ujumla. Kwa bahati mbaya leo hii Waislamu wanaonekana kuwa ni jamii ambayo haikuleta maendeleo kwa namna yoyote. Ukweli wa kihistoria umekuwa hauelezwi kuhusu ustaarabu wa Kiislamu na kwamba ndio uliokuwa kielelezo cha maendeleo ya wanadamu.

Mchango uliotokana na ustaarabu wa Kiislamu ama umekuwa ukihafifishwa au hauelezwi kabisa katika taarifa nyingi zinazotolewa. Kitabu hiki kimejaribu kuondoa tatizo hili kwa kuelezea ukweli wa kihistoria juu ya zama bora zilizotokana na mvuvumko wa Uislamu. Mchango mkubwa wa Waislamu katika sayansi, sanaa, na utamaduni unawekwa wazi kupitia kitabu hiki, pamoja na maelezo ya kina juu ya maendeleo ya kitaaluma ambayo yanatokana na dini ya Uislamu. Kitabu hiki kinatoa maelezo juu ya ustaarabu wa Kiislamu kwa muktadha wa tafiti mbalimbali kutoka kwa wasomi wa Kimagharibi.

Mafanikio ya ustaarabu wa Kiislamu na mchango wake kwa ulimwengu ndiyo uliophelekea mwamko wa Ulaya, mafanikio haya na mchango huu hujaelezwa kwa namna ipasavyo. Upofu huu unatokana na uhaba

wa tafiti, hali halisi ya Waislamu wa leo na kuoanisha kila kitu cha maendeleo na Ulaya. Maelezo juu ya ustaarabu wa Kiislamu yanagawika sehemu kuu mbili; sehemu ya kwanza ni ile ya wasomi wa sasa ambao wanakanusha mchango wa Waislamu kwa maendeleo ya Ulaya Magharibi. Sehemu ya pili ni kundi la wasomi wanaotambua mchango wa Waislamu kwa ustaarabu wa Kimagharibi. Kundi hili la wasomi limefanya kazi kubwa ya kubainisha hazina kubwa ya Waislamu katika kipindi cha zama za kati, wasomi hawa wameweka wazi kuwa mwamko na ustaarabu wa sasa wa Ulaya kwa kiasi kikubwa vimetokana na kazi iliyofanywa na Waislamu. Wanachuoni au wasomi hawa wanaelezea pia kuwa ustaarabu wa Kiislamu haukuwa wa kibubusa na wala haukuwabagua wasio Waislamu.

Hata hivyo, maelezo ya wasomi wa Magharibi yenye mrengo wa kisiasa, yamekuwa yakitilia mkazo juu ya matukio ya kigaidi kama lile tukio la tarehe 11 Septemba, 2001. Athari ya maelezo kama haya ni kutoonekana kwa mchango wa ustaarabu wa Kiislamu. Kuusoma au kuuelezea Uislamu kwa njia hii ni dhahiri picha ipatikanayo ni kuwa Uislamu ni dini ya vurugu na Vita. Kitabu hiki kupitia ushahidi wa historia, kimejaribu kuonesha makosa yanayotokana na kuusoma Uislamu kwa namna hii, na badala yake kinaelezea ni vipi Uislamu kama dini unavyohakikisha amani inakuwepo baina ya Waislamu na wasio-Waislamu. Jamii ya Waislamu katika kipindi cha zama za kati ilitafuta umoja kupitia mambo mbalimbali hata kukubali mchango wa wasiokuwa Waislamu, hivyo ni vyema kusoma ustaarabu uliopita, na kutumia maarifa hayo kujenga jamii yenye kuendelea.

SURA YA KWANZA



Nafasi ya Uislamu Katika Historia



Uislamu ndio ulioweka daraja kati ya ustaarabu wa Mashariki na ule wa Magharibi. Wasomi Waislamu ndiyo waliokuwa na elimu iliyoleta mwanga mpya katika nyakati tofauti. Katika hali ya ubunifu, Waislamu walitoa mchango mkubwa kielimu kwa muda mrefu. Waislamu walielewa kutafuta elimu kwao ni suala la lazima kwani ni wajibu wa kidini. Michango ya Waislamu inatokana na ukweli kwamba Uislamu ni dini inayoheshimu wanaadamu wote.

Uislamu umeweka bayana kuwa watu wote ni lazima wafurahie nema zilizomo ulimwenguni ndani ya maadili mema, na kufutilia mbali yale yote yanayofanya kundi moja la watu kuwa bora kuliko wengine. Uislamu unakwenda nje ya mipaka ya kijiografia kutoka Ulaya hadi Asia, na kwa hiyo, kuwa na umoja ndani yake wa jamii mbalimbali. Kupitia Uislamu hadhi ya wanawake nayo ilipanda sana. Mfumo wa maisha ya Kiislamu ndiyo uliopheleka chimbuko la ustaarabu wa Kiislamu katika maeneo yote.

Kwa muda wa zaidi ya miaka elfu moja, Uislamu ndiyo dini iliyokuwa ikiongoza kwa ustaarabu duniani. Lugha yake ya Kiarabu, ndiyo iliyokuwa lugha ya kimataifa na ya kisayansi¹. Hata hivyo Vitabu vingi vya historia huelezea kuwa mafanikio ya Uislamu yametokana na tamaduni mbalimbali. Wanahistoria wenye mtazamo huu wanataka kuonesha kuwa Uislamu hauna mchango wowote kwa ustaarabu wa

Kimagharibi na kwa hiyo ustaarabu wa Kimagharibi ni ustaarabu wa kipekee katika Zama za Kati². Maelezo yao yanaielezea historia ya Uislamu kuanzia karne ya saba na kuendelea, kwa kuishambulia dini hiyo, kitabu cha Quran na Mtume Muhammad (S.A.W). Wanahistoria wamejadili kwa upana historia ya Ugiriki na Urumi na hatua za mwanzo za maendeleo ya Ukristo, na kuelezea kwa kifupi zama za Uislamu, na kurukia mvuvumko wa Ustaarabu na Maendeleo ya Ulaya.

Waislamu waliiga tamaduni zilizotangulia na kujazia mchango wao na hatimaye kupelekea ustaarabu wa kipekee. Kwa upande mwingine, wale wasiokuwa Waislamu nao waliiga na kufuata desturi na taratibu za Waislamu. Uislamu vilevile umechangia maendeleo ya dini za Uyahudi na Ukristo, na kuweka misingi ya ustaarabu wa Kimagharibi.

SURA YA PILI



Elimu na Ustaarabu wa Kiislamu



Katika kutilia mkazo juu ya elimu na mafunzo³, Uislamu ulianza kwa kuziba ombwe la elimu lililokuwepo duniani katika karne ya saba. Mataifa makubwa yalianguka na Ulaya kuwa katika zama za giza, ambapo kupanuka kwa mipaka ya kijiografia kwa Uislamu kuliambatana na ukuaji wa elimu na utamaduni wa Kiislamu.

Qur-an imesisitiza sana umuhimu wa kujifunza. Neno ‘ilm’ limejitokeza mara 750 katika Qur-an, moja ya neno lililojitokeza mara nyingi katika Qur-an na Hadith za Mtume Muhammad (S.A.W). Zaidi ya hivyo Qur-an inaeleza bayana tofauti kati ya mwanadamu na viumbe wengine ni ule uwezo wake wa kudadisi⁴. Lugha ya Qur-an ni ya weledi wa hali ya juu katika kuelezea dhana za kisayansi na maeneo mengine ya kitaaluma. Lugha hii ya Qur-an inasomwa na kusikilizwa mara kwa mara na Waislamu. Lugha ya Kiarabu ambayo ndiyo msingi wa Uislamu na ustaarabu wake, inahitaji msukumo mkubwa kuliko ilivyopokelewa katika nchi za Magharibi.

Wakati wa zama za kati huko Ulaya, Kiarabu ndiyo lugha iliyotawala katika ulimwengu wa Kiislamu na ni lugha iliyokuwepo Ulaya. Lugha ya Kiarabu ilikuwa inatumika katika baadhi ya vyuo vikuu huko Ulaya mpaka pale kilatini kilipoanza kutumika kama lugha ya kufundishia. Kamusi na kanuni za nahau za lugha ya Kiarabu vilisaidia sana kupatikana kwa filolojia ya Kiyahudi.

Tangu awali, Waislamu walifahamu kuwa elimu ni katika mahitaji muhimu na makubwa, na kwa hiyo kuanzisha shule mbalimbali kwa ajili ya kutoa mafunzo wakati ambapo Ulaya elimu ilikuwa ni kwa watu maalum⁵. Jamii ya Waislamu ilikuwa ni jamii yenye muono mpana juu ya suala la elimu. Wanachuoni wa Kiislamu waliamini kuwa ujuzi, maarifa na ucha-Mungu ndivyo vyenye kustawisha maisha ya watu hapa duniani na akhera. Kutafuta elimu ni jambo lililosisitizwa katika Qur-an na Sunnah ya Mtume Muhammad (S.A.W).

SURA YA TATU



Kuanzishwa kwa Jamii ya Kwanza ya Kiislamu



Jamii ya kwanza ya Kiislamu ilikuwa ni ya watu waliokuwa tayari kujirekebisha iliwawe watu bora zaidi. Hivyo basi, walibadilisha mfumo wao wa maisha ili kwenda sambamba na Qur-an na Sunna. Qur-an na Sunna ndiyo vitu vilivyoathiri maisha yao katika hali zote. Kwa mfano, Qur-an inasisitiza juu ya umuhimu wa kufanya kazi kwa kuzingatia uasilia na kufurahia uzuri wa ulimwengu wa Mwenyezi Mungu. Uislamu umempa hadhi mwanaadamu na sio kumpachika dhambi ya kuzaliwa nayo au kurithi. Qur-an inauelezea mwili wa mwanaadamu kama ni muujiza ambao umevaa sifa za uungu⁶. Kwa kifupi, Mwenyezimungu amemtukuza na kumnyanyua mwanaadamu. Quran inasema, “Na hakika tumewatukuza wanaadamu” (17:70)

Pamoja na mafundisho mbalimbali ya Qur-an, Mtume Muhammad (S.A.W) ameonesha vilevile kivitendo udadisi na ubunifu. Mtume Muhammad (S.A.W) alizaliwa katika mji wa Makkah mnamo mwaka 570 B.K, akijulikana kama mtu mwaminifu na mkweli. Alipokea ufunuo (Wahyi) wa kwanza mnamo mwaka 610 B.K na kuanza kuwalingania watu wa Makkah, ambao walimtesa na hatimaye kuuhama mji huo na kwenda Madina. Tukio hili la kuhama ndilo lililopelekea mwanzo wa kalenda ya Kiislamu na kuasisiwa kwa jamii ya Waislamu. Baada ya Vita mbalimbali, Mtume Muhammad (S.A.W) na wafuasi wake walifanikiwa kuuteka mji wa Makkah na kuufanya kuwa kituo cha Uislamu. Dira ya Mtume Muhammad (S.A.W) ndiyo iliyoongoza ustaarabu huu mpya na

harakati za kufikia ufanisi bora. Msikiti ukawa ndio kituo cha kijamii, elimu na shughuli za kiserikali, mfumo wa kodi na uhisani uliasisiwa na kuendelezwa kwa shabaha ya kuwasaidia masikini.

Mtume Muhammad (S.A.W) alikuwa ni kiongozi mnyenyekevu ambaye aliishi maisha ya kawaida na alisisitiza kuwa watu wote, wakiwemo wanawake wana haki sawa. Kwa zama hizo, haya yalikuwa ni mafanikio makubwa, wakati ambapo watoto wachanga wa kike waliuliwa na baba zao kwa kuchelea aibu. Mtume Muhammad (S.A.W) ndiye aliyefundisha kwamba wanawake waendeleo kutumia majina yao hata baada ya kuolewa na sio majina ya waume zao waliowaoa. Wanaume waliwekewa ukomo katika kuoa na wanawake wakapewa haki ya kuacha, kupewa fidia⁷ na kusaidiwa kulea⁸ watoto. Wanawake waliruhusiwa kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kumiliki mali⁹. Haya yalikuwa maendeleo makubwa kwa wakati huo.

Kuenea kwa Uislamu sehemu mbalimbali duniani kulipelekea haja ya kuelewa sheria za Uislamu. Kwa muktadha huu madhehebu manne yaliibuka ambayo yameasisiwa na maimamu hawa: Abu Hanifa, Malik ibn Anas, Muhammad ibn Idris al-Shafi'i na Ahmad ibn Hanbali. Imam Abu Hanifa alitumia Qur-an kama msingi wa kujenga hoja za kisheria kwa madhehebu yake, na vilevile alijishughulisha na utafutaji wa Hadithi sahihi za Mtume Muhammad (S.A.W). Wanafunzi wake ambao waliibuka baadaye ndiyo waliobobea hasa katika fani ya sheria. Sheria ya Kiislamu iliimarishwa na kuasisiwa na kuwa ndiyo msingi wa ustaarabu wa Kiislamu.

SURA YA NNE



Ulimwengu wa Kiislamu



Ndani ya karne moja baada ya kuja Uislamu, Waislamu walifika Afrika ya Kaskazini na Hispania kwa upande mmoja na China na Indonesia kwa upande mwingine, huku ukiwavutia watu wengi wapya. Mwanzoni Waislamu walikabiliana na maadui zao kwa ari ya kushangaza, ukizingatia kwamba katika matukio mengi walikuwa wachache ukilinganisha na maadui zao.

Jambo lingine muhimu ilikuwa ni namna Waislamu walivyo ishi na wale ambao hawakuwa na uhasama nao. Wengi wa Wayahudi na Wakristo waliwakaribisha na Waislamu kwenye ardhi zao kwa sababu ya mateso na madhila yaliyowakuta kutoka kwa watawala wa dola ya Kirumi¹⁰. Waislamu hawakuwa na chembe ya ukatili, na Mtume Muhammad (S.A.W) aliwasihi kuwa wapole kwa watu wengine¹¹.

Waislamu hawakuharibu miji waliyoiteka, hawakuuwa au kuwafanya watumwa wa kiVita wanawake na watoto. Majeshi yao hayakutwaa miji badala yake walijenga mahema yao na vituo vya kijeshi pembezoni ya miji, baadhi ya maeneo haya yamekuwa miji maarufu, kama vile Cairo¹². Mji wa Baghdad¹³ ulitokana na kutanuka kwa shughuli za elimu na mafunzo na hatimaye kuwa mji maarufu kwa masuala ya kitaaluma. Watatu kati ya waanzilishi wanne wa madhehebu za kisheria waliishi na kufanya kazi za kitaaluma katika mji huu. Baghdad ndiyo uliokuwa mji mkuu wa dola ya Abbasiya, dola iliyotawala kwa muda mrefu katika

historia ya Kiislamu. Walikuwa ni Wamongoli walioharibu mji wa Baghdad na maktaba zake mnamo mwaka 1258 B.K.

Si kweli kwamba Uislamu ulienezwa kwa ncha ya upanga kama inavyodaiwa na baadhi ya watu. Waislamu walikuwa ni wachache katika nchi ambazo Waislamu walitawala kama vile, Iran, Iraq, Misri, Tunisia na Hispania¹⁴. Waislamu waliendelea kuwa ni wachache hata pale ambapo utawala ulikuwa wa Kiislamu katika nchi kama vile India na Sicily¹⁵. Kwa ujumla watawala wa Kiislamu hawakuwabughudhi wala kuwatesa Wayahudi, Wakristo na watu wengine walioishi kwenye mamlaka yao. Watu wengi waliingia kwenye Uislamu baada ya karne moja tangu Waislamu walipotwaa miji mbalimbali¹⁶. Uislamu uliingia Indonesia, nchi yenye Waislamu wengi duniani, bila ya Vita au nguvu bali ilikuwa kupitia wafanyabiashara na Masufi¹⁷.

Wakati Wamongolia walipotawala na kuharibu sehemu kubwa ya ustaarabu wa Kiislamu, watu hawa hawa ndio waliolingia kwenye Uislamu kwa hiari zao. Wafuasi wa Wamongoli ndio waliokuja na ustaarabu wa Kiislamu na utamaduni wake kwa namna yao.

Historia ipo bayana kwa namna Waislamu walivyowachukulia Wayahudi wakati wakiteswa na Wakristo kwa miongo kadhaa. Wayahudi ambao walikimbia mateso ya Wakristo walitafuta hifadhi katika miji ya Waislamu. Hispania, Waislamu waliwateua Wayahudi kuendesha au kusimamia maendeleo ya miji waliyokuwa wanaishi.

Katika nchi zingine za Waislamu, Wayahudi waliishi kama jamii na waliishi kwa mujibu wa mafundisho ya dini yao. Vilevile walishiriki katika shughuli za kiutawala na elimu katika taasisi za kitaaluma. Taaluma za dini na falsafa za Kiyahudi ziliendelea sana chini ya utawala wa Kiislamu. Hispania iliyokuwa chini ya utawala wa Waislamu ndiyo iliyokuwa kituo cha maarifa ya Uyahudi.

SURA YA TANO



Ustaarabu wa Kiislamu Ulaya na Asia ya Magharibi



Ulimwengu wa Kiislamu ulitanuka zaidi na kudhibiti hata maeneo ya bahari. Kwa karne nyingi, Waarabu walisafiri kwa kutumia meli na majahazi na walisafirisha bidhaa kutoka sehemu moja ya bandari hadi bandari nyingine. Waislamu waliendeleza ujuzi wao kuhusiana na mambo ya bahari na kuongeza usukani, ambapo ulimwengu wa Magharibi walikabiliana nao wakati wa Vita vya msalaba, na baadaye kuiboresha zaidi, astrolabu ambayo waliipata kupitia Wagiriki. Vilevile walipata sindano ya sumaku kupitia kwa Wachina¹⁸ na wakatengeneza dira ya kuongozea chombo.

Elimu ya bahari kwa Waislamu ilikua haraka kiasi kwamba kufikia kipindi cha Khalifa wa tatu, Uthman (R.A), jeshi la majini la Waislamu lilikuwa imara sana ambapo liliwapelekea Waislamu kudhibiti eneo la bahari ya Mediterania. Majahazi ya Waislamu baadaye yalikuwa yakisafiri kuelekea India na China hadi Pwani ya Afrika ya Mashariki kwa ajili ya biashara. Neno la Kiingereza “admiral” linatokana na neno la Kiarabu “amir” kwa maana ya kamanda au kiongozi.

Baada ya kuingia Hispania na Sicily, Waislamu hawakuendelea na juhudi zaidi katika kueneza Uislamu na kutwaa miji. Ustaarabu wa Kiislamu umeacha athari kubwa Sicily, katika sanaa, elimu na kilimo. Waislamu walitawala Sicily kwa miaka 200. Chini ya Mfalme Roger wa kwanza, utawala wa kisiwa hiki ulikuwa chini ya Waislamu na kuendelea

kuwa ni kituo cha utamaduni wa Kiislamu. Ujuzi wa Waislamu katika kutengeneza majahazi na boti ulisaidia Sicily kuwa sehemu inayoongoza katika masuala ya bahari wakati wa Mfalme Roger wa pili. Naye Mfalme Frederick¹⁹ wa pili alikuwa na uhusiano mzuri na Waislamu, watawala Waislamu ndio waliokuwa marafiki zake wa karibu, hali iliyopelekea awe na maadui Ulaya²⁰.

Wafanyabiashara Waislamu na mabaharia walisafiri sehemu mbalimbali duniani hali ambayo iliwasababishia wawe na mchango mkubwa katika elimu ya jiografia. Uislamu uliendelea kupanuka hadi Asia; India, kusini mwa Urusi na kusini Magharibi mwa China. Waislamu walibuni huduma za posta kwa ajili ya mawasiliano na sehemu hizi ambazo zilikuwa mbali na baadaye huduma hii iliboreshwa wakati wa dola ya Abbasiyah na Baghdad kuwa makao makuu ya dola hiyo. Maendeleo haya yalienda sambamba na mafundisho ya Quran na Sunna.

Popote pale ambapo Uislamu uliingia Waislamu waliishi na watu wa sehemu hizo na kujifunza baadhi ya mambo kutoka kwa watu hao na wao walifundisha ustaarabu wa dini yao, na kwahiyo Waislamu walileta ustaarabu wa maisha na namna ya kuishi na watu wengine. Athari ya Uislamu ilidhihiri katika miji mbalimbali duniani. Katika Asia ya Kati ambako misafara ya biashara ya Waislamu ilikuwa ikipita ilipelekea watu walioishi karibu na njia hizo kuingia katika Uislamu.

Waislamu walioishi Asia ya kati na hao Masufi ndio walioufikisha Uislamu kwa wale ambao waliishi mbali na njia za misafara ya kibiashara, na hatimaye Uislamu ukafika kaskazini na Mashariki ya Asia. Waislamu hawakubagua maeneo na kutenga maeneo ya vijijini na badala yake vijiji vilikuwa ni sehemu ya miji ya Waislamu. Walimu walikuwa ni watu muhimu sana katika kuwakutanisha watu wa miji mbalimbali. Utwaaji wa miji kwa Waislamu haukuwa kama ule wa dola nyingine, utawala wa Kiislamu haukuwa wa kiovu. Waislamu walistawisha miji kila pale walipoingia na kuishi, waliongeza biashara na elimu.

SURA YA SITA



Biashara



Waarabu walikuwa ni wafanyabiashara karne kadhaa kabla ya kuja kwa Uislamu, walivuna na kuuza ubani katika ukanda uliojulikana kama barabara ya ufukizaji ambayo ilipitia Maka. Waislamu walikuwa wafanyabiashara mahiri. Ukiacha Vita iliyopiganwa Misri na kaskazini mwa bahari ya Mediterania, biashara na ucha-Mungu ndivyo vilivyopelekea Waislamu na Uislamu kufika nchi za Afrika zilizo chini ya jangwa la Sahara, kwani Waislamu walijikita katika shughuli za biashara.

Hali hii ndio iliyochangia kuimarika kwa ustaarabu wa Kiislamu duniani. Muunganiko wa biashara, dini na utamaduni wa uwazi ndivyo vilivyochangia kwa Uislamu kuenea duniani. Wafanyabiashara Waislamu ndio hasa waliounganisha maeneo yaliyokuwa kwenye himaya za dola kubwa mbili za wakati huo, dola ya Kiajemi na ile ya Kirumi, na kuongeza ufanisi wa kibiashara katika maeneo hayo.

Waislamu walioishi sehemu mbalimbali duniani walileta fedha na vitega uchumi na kunyanyua sekta mbalimbali. Kwa hakika, wale wasiokuwa Waislamu walinufaika na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Waislamu, hata katika maeneo ya vijijini. Ni dhahiri chini ya Waislamu, watu waliishi maisha bora kuliko ilivyokuwa chini ya dola za Kiajemi na Kirumi. Biashara ilikuwa na hadhi ya kijamii katika miji ya Waislamu. Wafanyabiashara walichangia kiasi kikubwa katika maendeleo ya

kitaaluma na waliweza kuwapeleka watoto wao kwenye vyuo vikuu, na wale waliokuwa wataalam waliheshimiwa kwa kiasi kikubwa. Kufuatia ujio wa Uislamu, misafara ya biashara ya marashi ililindwa kwa amri za kisheria za Quran na baadae ilikuja kuwa misafara ya hija²¹. Biashara ilikuwa ni muhimu sana kwa Waislamu, bidhaa mbalimbali ziliuzwa na kununuliwa wakati wa Hija, kwa namna hii mji wa Makkah ukawa ni mji wa kidini wenye amani na kituo cha biashara cha kimataifa.

Kwa upande wa Afrika, Waislamu waliongeza biashara kwa kiasi kikubwa, mara nyingi wakipitia Sahara na kupelekea kuenea kwa ustaarabu wa Kiislamu katika bara la Afrika. Njia za misafara ya biashara zilianzia Magharibi mwa Sahara hadi Afrika ya Mashariki. Uislamu ulienea kupitia biashara kiasi kwamba zaidi ya nusu ya wakazi wa Afrika walikuwa ni Waislamu, ilikuwa ni lugha tu ambayo ilitenganisha miji katika bara hili. Kuingia kwa Uislamu katika bara la Afrika kulileta tofauti kubwa katika biashara kwani ndani ya muda mfupi Waafrika nao wakawa washiriki wazuri katika biashara. Bandari zilizokuwa karibu na bahari ya Mediterania ziliendeshwa kwa ajili ya kufanya biashara na Ulaya na kuunganisha na njia mbalimbali za misafara ya biashara.

Kama ilivyokuwa kwa Afrika, ndivyo hivyo Waislamu walivyoingia China. Wafanyabiashara wengi waliishi China na kupelekea kuwepo kwa idadi ya kutosha ya Waislamu, hali hii ilipelekea kwa baadhi ya watu wa China kuukubali Uislamu na hatimaye kukubaliwa na watawala wa dola ya Mongolia. Waislamu walitumia njia nyingine ya misafara ya biashara, iliyojulikana kama “Barabara ya hariri”, ambayo ilikuwa ikitumika kwa ajili ya kusafirishia hariri kutoka China. Wafanyabiashara Waislamu waliimarisha njia hii na kufanya kuwa salama zaidi, wakati huohuo wakipitia bahari iliyokuwa ikitumiwa kwa ajili ya biashara kati ya Uajemi na China. Njia hii ilikuwa ikitumika hata kabla ya Uislamu. Kwa upande wa nchi kavu, Waislamu kwa mara ya kwanza walikutana na Wachina upande wa Magharibi ya China. Katika mji wa Canton, idadi ya Waislamu iliongezeka na kupelekea kupatiwa jaji wa kusimamia sheria za Kiislamu.

Biashara iliongezeka kati ya Wachina na Waislamu, na Wachina kunufaika kutokana na ujuzi waliokuwa nao Waislamu kwenye masuala yanayohusiana na elimu ya bahari na vyombo vya utafiti baharini. Kwa misafara ya biashara iliyotumia njia za mansuni kupitia India na China kuna mifano mingi ya kuthibitisha uhusiano mzuri baina ya Waislamu

na jamii zilizoishi sehemu hizo. Waislamu ndio waliounganisha China na Ulaya Magharibi, hivyo kuwarahisishia wafanyabiashara wa kutoka Mashariki ya Mbali kusafiri katika hali ya usalama zaidi kwa kupitia bahari ya Mediterania mpaka Hispania²² iliyokuwa chini ya Waislamu. Njia hii ya kibiashara iliendelea kutumiwa hata nyakati za Vita kama vile wakati wa Vita vya Msalaba. Biashara ya Waislamu ilineemesha bara la Ulaya, na kusaidia bara hilo kubadilika kutoka kwenye biashara ndogo mpaka sehemu ya biashara ya kimataifa. Hali hii pamoja na elimu iliyopatikana kutoka kwa Waislamu ndio iliyopelekea mvuvumko (mwamko) wa ustaarabu wa Ulaya.

SURA YA SABA



Kilimo na Tekinolojia



Kilimo kilikuwa ni sehemu muhimu kwa biashara za Waislamu na vilevile kilipelekea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na kiutamaduni katika ulimwengu wa Kiislamu. Historia hii inaeleweka kwa ufinyu sana katika nchi za Magharibi, hii ni kutokana na upotoshwaji wa makusudi dhidi ya Uislamu. Kwa hakika, Waislamu walikuwa ni weledi katika kilimo na walisaidia kuongeza mazao ya kilimo yaliyokuwepo na kuleta mazao mapya kama vile majani ya kulisha ng'ombe, alfalfa. Aidha, Waislamu walifanya mabadiliko makubwa katika kilimo yaliyopelekea kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao na kuimarika kwa uchumi. Ubunifu wao ndio uliosababisha kuongezeka kwa mavuno, matumizi bora ya ardhi na kuimarisha mfumo wa umwagiliaji. Athari kubwa ilikuwa katika uzalishaji wa matunda, mbogamboga, mpunga, nafaka, miwa, mawese na pamba²³.

Waislamu walipeleka Hispania bidhaa za kilimo na njia za uzalishaji, hii ilipelekea kukua kwa uchumi wa nchi hiyo na kuongezeka kwa mauzo ya nje. Ilikuwa ni Waislamu waliopeleka Hispania matunda yenye asili ya Asia, kama vile madaransi, ndizi na maembe, hadi upande wa Magharibi wa nchi hiyo. Walieneza kilimo cha matikiti maji na aina tatu za mboga mboga ambazo hazikuwepo nazo ni: spinachi biringanya na nyanya chungu. Waislamu walichangia kusambaa kwa kilimo cha bidhaa za chakula kama vile ngano, shayiri na mpunga na aina nyingine za mazao na kuimarisha shughuli za kilimo. Tambi ilikuwa ni sehemu ya bidhaa

zilizofikishwa Italia na Waislamu²⁴. Waislamu waliongeza matumizi ya mchele, na hatimaye kuwa chakula kikuu, aidha walipeleka zao la nazi na tende upande wa Magharibi. Ushahidi madhubuti wa kilugha unaashiria kuwa Waislamu walipeleka sukari Ulaya Magharibi, kwani neno la Kiingereza ‘Sugar’ linatokana na neno la Kiarabu ‘Sukkar’.

Kwa upande wa viwanda, Waislamu walianzisha na kuendeleza viwanda vya nguo. Neno ‘Cotton’ (pamba) linatokana na neno la Kiarabu na zao la pamba ndio muhimu kwa viwanda vya nguo. Zao hili lililimwa sana katika miji ya Waislamu na mji wa Baghdad ulikuwa ni kituo kikubwa cha uzalishaji wa zao hili.

Mazao ya kilimo yalikuwepo Asia na Afrika karne nyingi kabla ya kuja Uislamu, lakini kupitia Waislamu mazao haya yalifika sehemu ambazo hayakuwepo kabla. Kama ilivyodhihiri, Uislamu ulileta maendeleo kwa mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla.

Dola ya Kiislamu ilirahisisha usafiri wa watu na bidhaa na kurekebisha mambo kadhaa ya kikanuni ili kurahisisha biashara mambo hayo ni kama vile, pesa ya pamoja, vipimo na mizani na kuimarisha mitandao ya mawasiliano. Wahandisi Waislamu waliendeleza mfumo wa umwagiliaji na teknolojia nyingine zinazohusiana na saa, mashine za upepo, vinywaji, utengenezaji wa vioo, mafuta mazuri, mazulia na aina nyingine za bidhaa. Kwa hakika, dola ya Kiislamu iliathiri kwa kiasi kikubwa maisha ya Wazungu, Waafrika, Waarabu na Waasia kwa karne nyingi. Mafanikio yaliyotokana na ustaarabu wa Kiislamu yalipelekea kukua kwa uchumi. Urafiki wa kibiashara, ulitoa fursa kwa bidhaa, maarifa, elimu na lugha ya Waislamu kufika sehemu tofauti za dunia.

SURA YA NANE



Ustawi wa Elimu ya Uislamu



Kadiri jamii ya Waislamu ilivyoendelea kukua, ndivyo hivyohivyo elimu nayo iliendelea kukua hasa katika kipindi cha Ukhalifa wa Abbasiyya. Katika kipindi hiki Waislamu walianza kuandika Vitabu, hasa kuhusiana na masomo ya Quran na dini nyingine pamoja na sira ya Mtume Muhammad (S.A.W). Katika kipindi hiki kazi za tafsiri kwa lugha ya Kiarabu kutoka lugha mbalimbali, kama vile Kigiriki na Kiajemi, zilishamiri. Lugha ya Kiarabu ilikuwa ndiyo lugha ya kufundishia katika vyuo vya Ulaya Magharibi, na lugha kama ya Kiajemi iliathiriwa na maneno ya lugha ya Kiarabu.

Taasisi za elimu na maktaba kama ile ya Jundishapur iliyopo Iran ziliongeza ujuzi na utaalamu katika zama hizi za Waislamu, hata watu walikuwa na maktaba zao binafsi. Khalifah al-Hakam wa pili wa Hispania alikuwa na Vitabu 400,000 kwenye maktaba yake. Taasisi za Elimu ya juu kama vile Chuo Kikuu cha Al-Azhar cha Cairo, viliandaa mifumo ya kitaaluma ambayo inatumika hadi hivi leo, hasa katika nchi za Ulaya Magharibi.

Khalifa Harun Al-Rashid alikuwa ni Khalifa wa kwanza kuwa kiongozi wa dola mwenye hadhi ya uongozi wa kidunia. Kipindi cha utawala wake, mji wa Baghdad ulipata umaarufu wa kuwa ndiyo moyo wa kilele cha mafanikio ya Uislamu. Umaarufu wa Khalifa Harun Al-Rashid

duniani ulipelekea ajulikane kama ni mtu muhimu katika bara Arabu. Baada ya kusoma kwa walimu mbalimbali, mtoto wa Khalifa Harun Al-Rashid na ambaye alikuwa mrithi wake, Al-Ma'mun alikuwa ni bingwa katika sharia, fasihi, falsafa, tenzi na sayansi. Wakati wa utawala wake, Khalifa Al-Ma'mun aliasisi kituo cha elimu ambacho kilijulikana kama "Nyumba ya Hekima" katika mji wa Baghdad, kituo ambacho kiliwavutia wanachuoni kutoka sehemu mbalimbali duniani na baadaye kituo hiki kikawa maarufu katika mambo ya utafiti, elimu ya anga na ukalimani kwenda lugha ya Kiarabu. Kazi za Kigiriki zilizotafsiriwa katika lugha ya Kiarabu hatimaye ziliingia Ulaya ya Latini (Latin Europe); na kuhamasisha mwamko wa ufuatiliaji wa kazi za Aristotle na wanafalsafa wengine wa Kigiriki. Katika kipindi hiki cha tafsiri, hapakuwepo na mtu yeyote kutoka Ulaya Magharibi ambaye angeweza kufanya kazi hii au kuzungumzia, aidha hapakuwepo na kitu kilichojulikana kama "Ugiriki ya Kale".

Wanawake nao walijizatiti katika kujifundisha fani mbalimbali za Quran, sheria, teolojia, sanaa na tiba. Wakunga walihitajika sana japokuwa wanawake Waislamu walibobea katika taaluma nyingine za tiba. Wanawake waliheshimiwa kwa kuwa na utaalamu wa fani mbalimbali. Nafasi 17 za utawala na uendeshaji wa dola zilishikwa na wanawake, wanawake 9 walikuwa ni walumbi, 4 walijenga misikiti na taasisi nyingine za umma. Wanawake 42 walikuwa ni wataalamu wa teolojia, 23 wanamuziki, na 76 washairi. Wake wa Makhalifa walishindana katika kutunga na kuandika mashairi²⁵.

Imam Al-Ghazali ni mfano wa elimu iliyokuwepo wakati huo, ambaye alikuwa ni mwanachuoni nguli katika teolojia ya Kiislamu. Ibn Khaldun, muasisi wa elimu ya jamii na masomo ya sayansi ya jamii, naye ni mfano mwingine wa ubora wa elimu ya wakati huo. Arnold Toynbee anaelezea kitabu cha Ibn Khaldun, al-Muqaddimah, kama ni kitabu cha falsafa ya historia na kwa kweli ni kazi kubwa ya namna ya kipekee²⁶. Mtazamo wa Ibn Khaldun ni mpana, kazi yake inaelezea maumbile mpaka matukio yaliyopita, ikijumuisha matukio yaliyomo ndani ya Biblia, katika jamii za Kiajemi, Kigiriki na Kirumi na hata historia ya Waarabu.

Utumiaji wa lugha ya Kiarabu katika vyuo vikuu vya Ulaya Magharibi uliendelea kama ilivyokuwa kabla, hasa katika kituo cha elimu na mafunzo cha Cordoba. Kuwa msomi kwa watu wa Magharibi kwa wakati huo ilikuwa ni jitihada binafsi na wasomi wengi waliachana

na taasisi za elimu zilizokuwa chini ya udhibiti wa kanisa. Ubora na uzuri wa ustaarabu wa Kiislamu unaonekana katika kutumia elimu na ujuzi unaotokana na tamaduni nyingine, Uislamu ulikuja na mtazamo wa kisomi na kutoa mchango mkubwa wa elimu duniani. Elimu na mafunzo yalikuwa ni mambo ya kawaida kwa jamii ya Waislamu.

SURA YA TISA



Sayansi



Qur-an inaelezea kwa kina kuhusiana na maumbile asilia na uwepo wa miujiza ya Mwenyezi Mungu ulimwenguni. Zipo aya nyingi za Quran zinazotoa maelezo juu ya maumbile ya asili na sayansi na kuonesha uhusiano wake na maumbile ya Mwenyezi Mungu, na hata kuhimiza tafiti za kisayansi²⁷. Qur-an inawataka watu kuelewa ulimwengu kupitia ushahidi yakinifu, aidha Qur-an inazungumzia juu ya takdiri, au vipimo; uwiano baina ya ujazo na ubora bila ya kuwacha kimojawapo²⁸.

Mwanzoni kabisa wanachuoni wa Kiislamu tayari walishatambua kuwa dunia ni mviringo kwa kufuata maelezo ya Qur-an. Hata baada ya mvuvumko wa Ulaya, bado watu wa Ulaya walikataa kukubali kuwa dunia ni mviringo na kung'ang'ania kuwa dunia ni tambarare²⁹. Hispania iliyokuwa chini ya Waislamu, wanaanga wa Kiislamu na wale wa Kiyahudi walikataa nadharia za Ptolemy tangu mwanzoni na walikubaliana na maelezo yalitolewa na Aristotle. Wanaanga Waislamu walisahihisha nadharia za Ptolemy ili kuwiana na shajara ya Kiislamu na walitambua kuwepo kwa mfumo mwingine wa kisayari³⁰. Waislamu walikwishajua namna ya kupata mzingo kwa kutumia pai hata kabla ya kujua juu ya jometri ya Kigiriki.

Waislamu walipoziteka dola za Warumi na Waajemi walizihifadhi na walizienzi taasisi za kisayansi. Junershapur ndicho kilichokuwa kituo

cha masuala ya kisayansi katika ulimwengu wa Kiislamu na wataalamu wake walitoka Damascus mji mkuu wakati wa dola ya Bani Umayyah. Sayansi ya Kiislamu ilitawala duniani kwa karne nyingi na kustawi zaidi wakati wa utawala wa Abbasiyyah. Wasomi kutoka India, Urumi na Uajemi walifika Baghdad kujifunza fani tofauti kutoka kwa wanachuoni wa Kiislamu. Mada zote ziliandikwa kwenye lugha mpya ya kisayansi. Mada zote zilitafsiriwa katika lugha ya Kiarabu kabla ya kufafanuliwa, ambayo ilipelekea kuibuka kwa misamiati mipya na ubunifu mkubwa.

Maendeleo katika elimu ya anga yalisaidia sana kwa wasafiri, ambao walihitaji kujua mwenendo wa sayari na nyota kwa lengo la kujua njia zipi za kufuata na kwa muda upi. Mwezi nao ulikuwa ni muhimu kwa maisha ya Waarabu, ambao walizigawa nyota katika makundi 28 yajulikanayo kama misimu ya mwezi. Mwezi ndio unaoambatana na misimu ya mwaka³¹. Waislamu walifundisha kuwa dunia ina umbo la tufe. Fani ya kemia iliendelea karne moja na nusu baada ya kuja kwa Uislamu. Waislamu walichangia kiasi kikubwa katika hisabati ikiwa ni pamoja na logarithimu ya Muhammad ibn Mussa na maeneo ya Aljebra, Jometri, vipimo vya digrii na trigonometriki³². Harakati za kutafsiri kazi mbalimbali zilihamasishwa na wataalamu wa Kiislamu, kazi hizi zilichangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya sayansi na kuwa chimbuko la mwamko wa maendeleo Ulaya.

SURA YA KUMI



Tiba



Miaka ya mwanzoni ya Uislamu, Uchina, Ugiriki na Uajemi ndizo dola zilizotawala katika uwanja wa tiba. Wasomi wa Kigiriki walikaa Junelshapur ambapo kulikuwa na kituo kikubwa cha mafunzo na elimu, sehemu ambayo imezalisha madaktari wengi wa Arabuni na Uajemi.

Taaluma ya tiba imechangiwa kwa kiasi kikubwa na Mtume Muhammad (S.A.W) ambaye ametoa ushauri mbalimbali juu ya maradhi kadhaa, ulaji unaozingatia afya bora. Kwa hakika walikuwa ni Waislamu ambao waliendeleza fani ya tiba. Hunayn ibn Is-haq aliyeishi karne ya tisa (9), alitafsiri kazi nyingi kutoka kwenye lugha ya Kigiriki kwenda lugha ya Kiarabu, vile vile aliandika Vitabu vingi katika fani ya tiba, Vitabu ambavyo vilileta athari kubwa katika fani ya tiba aidha daktari huyu alikuwa ni mwalimu wa madaktari wengi walioleta mageuzi makubwa katika fani ya tiba.

Katika zama za utawala wa Abbasiya, wengi walijifunza taaluma ya tiba na wengi wao wakawa madaktari. Mazingira yalikuwa muafaka kwa maendeleo ya elimu na wasomi waliheshimika kwa kiasi kikubwa. Mwanzoni mwa karne ya 9 mji wa Baghdad ulikuwa na wataalam wa tiba (madaktari) 860 wenye leseni za kutoa matibabu, palikuwepo hospitali nyingi na shule³³. Katika kipindi hiki muhimu kwa maendeleo ya tiba katika historia ya Kiislamu, wanapatikana ndani yake

wanachuoni watatu ambao ni; Al-Razi, Al-Majust na Ibn Sina, kazi za Al-Razi zinaashiria ukomavu na ubora wa tiba za Kiarabu, na mchango wake mkubwa katika fani ya tiba ni pale alipotofautisha magonjwa ya tetekuwanga na surua. Aliandika Vitabu zaidi ya mia mbili, nusu ya hivyo ni juu ya tiba, ikiwa ni pamoja na kuandika kitabu chenye juzuu kumi kuhusiana na tiba za Kigiriki. Abu Ali Al-Husayn ibn Sina (Avicenna) alikuwa ni mwanachuoni maarufu katika falsafa. Maendeleo ya taaluma ya tiba za Kiislamu yalikuwa na mafanikio makubwa kupitia kazi zake mfano ni kitabu chake cha Al- Qanun Fil -Tibb, kinachojulikana katika ulimwengu wa Magharibi kama “the Qanun”, ambacho kipo kwenye juzu tano³⁴.

Mwanzoni mwa Uislamu kule Hispania, wasomi waliotaka kujua tiba walikwenda Baghdad, Cairo, Damascus, na Iran kujifundisha fani ya tiba katika vyuo vikuu na hospitali. Baadaye Waislamu wa Hispania walianzisha vyuo vyao vikuu na vituo vya tiba na falsafa, hali iliyopelekea wimbi la wataalamu wa Kiislamu kuelekea Ulaya mnamo karne ya kumi na mbili. Mwanachuoni maarufu wa kutoka Andalusia, alikuwa ni ibn Rush (or Averroues). Huyu ni mwanachuoni aliye acha athari kubwa Ulaya Magharibi kupitia falsafa,vile vile alikuwa ni jaji, daktari, na mtunzi wa kamusi ya elimu ya tiba.

Edward Browne ameandika kwamba Waislamu wenye asili ya Kiarabu na wasio na asili ya Kiarabu walitoa mchango mkubwa katika elimu ya dhana za sayansi ambayo wameipokea kutoka kwa Wagiriki kuhusu kemia na tiba. Hatimaye Waislamu waliona kuwa kemia na elimu ya mimea (botany) kuwa ni muhimu sana kwa kuandaa dawa na elimu hizo haziwezi kusomwa kando na tiba. Elimu ya tiba (medical) na madawa (pharmaceutical) ilienea katika ulimwengu wote wa Kiislamu kama zilivyofundishwa na wanachuoni wa Kiislamu ambao walisafiri sehemu mbali mbali kujifunza taaluma hizi. Waislamu walijulikana kwa hospitali zao na ndio walikuwa wa mwanzo kuvumbua mfumo wa uendeshaji hospitali kama ilivyo leo. Zaidi ya uvumbuzi katika madawa, wataalamu wa Kiislamu walikuja na misamiati ya kitiba na namna ya taratibu za kuandaa matibabu.

SURA YA KUMI NA MOJA



Fasihi ya Kiarabu



Fasihi na sanaa zimekuwa nyanja muhimu katika ustaarabu wa Kiislamu. Ubunifu wa Waislamu ulinyanyua na kuleta mafanikio makubwa kwa Waislamu na wasiokuwa Waislamu. Msingi wa fasihi ya Kiislamu ilikuwa ni lugha ya Kiarabu na matumizi yake. Kila utamaduni una muundo wake, ishara zake, pambo zake, tashibiha ndivyo ilivyo kwa utamaduni wa Kiislamu.

Fasihi ya Kiislamu inadhihirisha mila na desturi za Muislamu na sifa zake zinazomtofautisha na mila na desturi zilizokuwepo kabla ya Uislamu kwenye maeneo kama vile, ushairi, tenzi, hekaya na simulizi za makabila zilizokusanya maisha ya watu maarufu. Mwanahistoria maarufu Ibn Khaldun anatueleza kuwa kitabu kinachohusu sanaa ya masuala ya muziki cha Abu al-Faraj kimekusanya yale yote ambayo Waarabu waliyapata kama mafanikio katika mashairi, historia au simulizi, muziki, n.k³⁵

Wahusika wakuu wa fasihi kabla ya kuja kwa Uislamu walikuwa ni wafalme na mashujaa wa makabila yao. Kuimba mashairi ya kuwasifu mashujaa wa jangwani ilikuwa ni sehemu ya utamaduni. Waarabu walithamini sana mashairi maarufu ya Muallaqat (The Seven Odes)³⁶. Waarabu wengi hadi leo bado wanakumbuka na kusoma kitabu hiki chote. Quran haikuwazuia washairi wa Kiislamu kutumia ujuzi wao katika fani hii, hata katika zama za Mtume Muhammad (S.A.W). Bali, katika kipindi cha Makhalfu wanne wa kwanza walionesha shauku kubwa katika mashairi kwa kuzingatia maadili ya Uislamu³⁷. Kipindi

cha Banu Umayyah kulikuwa na ubunifu mkubwa katika fani ya mashairi na lugha.

Kulikuwa na maendeleo makubwa katika uandishi wa nathari au hadithi ingawa simulizi ilikuwa ndio njia hasa ya kujieleza. Simulizi kuhusu watu maarufu ziliandikwa ingawa sehemu kubwa ilihusu juu ya historia. Simulizi zilizokuwa maarufu zilihusu masuala ya Vita za mwanzoni mwa Uislamu. Kitabu kikubwa katika taaluma hii ni sira ya maisha ya Mtume Muhammad (S.A.W) iliyoandikwa na Ibn- Ishaq kupitia mahojiano na watu waliomjua Mtume Muhammad (S.A.W) miongoni mwa jamaa zake na Maswahaba. Njia yake ya silsila mpaka wakati wa Mtume Muhammad (S.A.W) ndiyo iliyotumika vilevile katika kukusanya hadithi.

Nathari nyingi, kama vile uandishi wa mashairi marefu, yaliandikwa kipindi cha miaka 500 ya zama za Abbasiya na kuendelea kupitia utaratibu wa kitaalamu zaidi uliosimamiwa na Khalifa. Ni muhimu kutofautisha kati ya zama za uandishi wa fasihi wakati wa Banu Umayyah na ule wa Abbasiyah, hasa katika nusu ya kwanza, ambapo palikuwepo mabadiliko makubwa katika fasihi, falsafa, sayansi na sanaa. Nathari ilitawala, ingawa fani ya ushairi bado ilikuwa na hadhi kubwa, hii ilitokana na muingiliano na tamaduni nyingine, hasa Waajemi. Rejea nyingi zilitafsiriwa kutoka lugha ya Kiajemi na kuongezewa rejea za Kiarabu na kuwa sehemu ya kujifundisha historia ya Uislamu. Utaratibu huu ulikuwa na athari kubwa kwa upande wa uandishi wa simulizi.

Miongoni mwa kazi zote za fasihi za kipindi hiki cha awali, iliyokuwa maarufu na kupendwa kuliko zote ni mkusanyiko wa hadithi za “Alfu lela Ulela”. Hadithi nyingi katika hizo zilikuwa zimetafsiriwa kutoka kwenye Kiajemi zikichanganywa na hadithi na nyimbo za Waarabu na kuwa hazina ya hadithi za kufundishia Waislamu. Mchakato huu uliathiri mpangilio wa hizo hekaya na maana ya ndani ya hekaya hizo³⁸.

Shauku kubwa katika uandishi wa nathari ilipelekea kuibuka kwa namna mpya ya utunzi uliojulikana kama maqamat, aina ya uandishi ambayo haigusii tukio moja kwa moja. Maqamat ya Ahmad al-Hamadhani inadhaniwa kuwa ni kitabu kilichoandikwa kwa weledi mkubwa wa lugha ya Kiarabu baada ya Quran³⁹. Wakati wa kipindi cha Abbasiyah, mashairi yenye maelezo ya kina, mbinu na muundo bora yalitapakaa kuliko ilivyokuwa kabla ya utawala huu wa Abbasiyah.

SURA YA KUMI NA MBILI



Fasihi ya Kiajemi



Iran ni mchangiaji mkubwa wa ustaarabu na utamaduni wa Kiislamu nje ya ulimwengu wa Kiarabu. Wanachuoni mbalimbali wenye asili ya Iran ni sehemu ya historia ya ustaarabu wa Kiarabu kwani waliandika rejea zao kwa lugha ya Kiarabu. Baada ya kufufuliwa kwa lugha ya Kiajemi, fasihi ya Kiajemi iliibuka na kuwa na umaarufu mkubwa. Kipindi cha matumizi makubwa ya lugha ya Kiajemi kilikuwa ni muhimu sana kwa historia ya Iran na utamaduni wa Kiislamu. Kazi za mfano wa mashairi ya al-Rumi, Sa'di na Hafiz, ambazo zilitafsiriwa katika lugha mbalimbali na kuthaminiwa na watunzi tofauti maarufu wakiwemo wale wa Ulaya Magharibi.

Ingawa Kiarabu na Kiajemi zote ni lugha tajiri, mwanzoni mwa Uislamu sehemu kubwa ya fasihi ya Kiarabu ilikuwa kwa njia ya simulizi, wakati lugha ya Kiajemi ilishakuwa na rejea za kutosha kupitia maandishi, ikiwa ni pamoja na mashairi yaliyoandikwa kwa urefu, mtindo ambao baadaye ukawa ni sehemu ya fasihi ya Kiislamu. Ujio wa Uislamu ulibadilisha lugha ya Kiajemi kwa kuingiza maandishi ya Kiarabu na nyongeza ya matamshi. Quran na lugha ya Kiarabu vimeongeza msamiati⁴⁰ zaidi katika lugha ya Kiajemi. Waislamu, hasa wakati wa Abbasiyah, waliiga na walichangia maendeleo ya utamaduni wa Iran.

Wakati Wairan walitafsiri kazi mbalimbali kutoka lugha nyingine kwenda Kiarabu, Waarabu waliwaongezea Wairan baadhi ya misamiati

ya lugha ya Kiarabu na ile ya Uislamu na muundo wa uandishi wa mashairi. Qasida za Kiarabu zilitumiwa sana na Waajemi na kupelekea Waislamu kuwa na namna tofauti ya muziki. Muundo mwingine wa mashairi wa Wairan ambao unatokana na ubunifu wa Umar al-Khayyam ulikuwa ni ule wa tarbia, ambao umetafsiriwa katika lugha ya Kiingereza. Ingawa kazi hii ina mistari michache, minne, ilikuwa ndiyo chimbuko la mashairi ya Kiajemi.

Kufikia karne ya 15, lugha ya Kiajemi na fasihi yake ilisambaa India na kuathiri lugha na fasihi ya Waislamu walioishi huko. Hali hii ilipelekea kuibuka kwa lugha mpya ya India iliyojulikana kama Urdu, ambayo ilitokana na Indo-Aryan. Pamoja na lugha mbili hizi, Mughal (Waislamu wa India) walikuwa na ustaarabu wao ambao nao uliathiri fasihi ya Kiajemi. Lugha ya Kiajemi na fasihi yake ilichangia kwa kiasi kikubwa utamaduni wa Kiislamu kwa upande wa sanaa.

SURA YA KUMI NA TATU



Sanaa



Minara miwili inayopendeza sana iliyopo Hispania ni kielelezo cha ufanisi wa sanaa ya Kiislamu: Msikiti mkubwa wa Cordoba na Alhambra kule Granada. Majengo haya yenye mvuto na ambayo yanaonesha utaalumu mkubwa wa elimu ya usanifu waliyokuwa nayo Waislamu. Quran inasisitiza mno juu ya dhana ya uzuri⁴¹. Waislamu walipendelea kuona dhana hii ya uzuri inajitokeza katika kila wanachokifanya ili kiwe chenye kuvutia.

Waislamu walikuwa ni mafundi hata katika kazi za mikono, hasa katika utengenezaji wa mazulia, ambayo yalisababisha ongezeko katika uzalishaji wa malighafi, mazuria yalitumika misikitini na hata wasafiri kama sehemu ya vifaa vya nyumbani. Mazulia yalitumika sana kwa ajili ya kusalia maeneo yote Waislamu walipokuwa. Mwanzoni mwa mwamko wa maendeleo Ulaya, mazulia yalikuwa ni sehemu ya bidhaa zilizohitajika sana katika nchi za Ulaya na kuagiziwa kutoka miji ya Waislamu. Bidhaa hizi zilithaminiwa kwa namna ilivyotengenezwa kwani ilijumuisha mapambo ya aina tofauti.

Upande wa ufinyanzi na vioo, Waislamu walivumbua teknolojia ya ufuaji wa chuma, ambayo ilipofika Ulaya ikawa inatumika kama njia mojawapo ya kuibuka kwa “ufinyazi wa Kimagharibi”. Aidha walikuwa ni Waislamu ambao walivumbua matumizi ya vioo vya

yabisi kutengeneza ming'aro na vyungu mbalimbali vya rangi. Mbinu ya ming'aro ya Kiislamu iliingia Ulaya kupitia Hispania na Italia. Italia ilikuwa ikinunua vyungu vya vioo, na sahani za ufinyanzi kutoka kwa Waislamu kwa ajili ya kupamba makanisa yao kwa kipindi cha karne tatu. Waislamu walizalisha bidhaa za vioo na kazi za kokoto kwa kiasi kikubwa na kwa ufanisi. Bidhaa za vioo zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mapambo.

Sanaa ya muziki imekuwepo toka mwanzo mwa Uislamu na kudumu katika kila miji ya Waislamu ukiwemo mji wa Hijaz ambao ndio chimbuko la Uislamu. Waislamu waliipokea sanaa hiyo ya sauti ⁴² na pia Mtume (s.a.w) alitia mkazo usomaji wa Quran kwa sauti nzuri. Muziki huko nyuma wakati wa Makhhalifa wa mwanzo ulijikita katika sauti. Uboreshaji ulikuwa zaidi kwenye visomo, ikisisitizwa sauti tu bila maneno. Muziki ni asili ya utamaduni wa watu na Waislamu hawakuzuia desturi za watu waliowakuta katika miji, hivvyo muziki haukuguswa. Sauti ya muziki wa mahali ni ushahidi wa wazi kwenye utamaduni wa nyimbo za wenyeji, mapigo na vifaa vyake.

Aidha kwa kutumia rangi mbali mbali za kuvutia na vito, Waislamu waliasisi sanaa ya uchoraji katika majengo, mazulia na hata kwenye mavazi. Sanaa ya uchoraji, kama usanifu majengo, ilikuwa na umuhimu mkubwa katika ulimwengu wa Kiislamu. Nakala za mwanzo za Quran ziliandikwa kwa maandishi yenye nakshi za kupindapinda na maandishi ya Quran yaliyosanifiwa Maka na Madina katika karne ya kwanza ya Uislamu kwa kuanzisha sanaa ya kaligrafia⁴³.

Aina tofauti za maandishi zilitumika katika tasnia ya habari na upambaji majengo. Waislamu walifanya kila kitu kwa lengo la kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu, ni mwelekeo huu ambao ulioathiri tabia zao. Uweledi wa Waislamu, hasa wale wa mwanzoni mwa historia ya Uislamu, ambao walikuwa waanzilishi, unaonekana hasa katika maendeleo ya elimu ya maumbo katika mapambo. Msikiti unakusanya sanaa nyingi za Waislamu, hasa sanaa ya uandishi hati na mapambo. Usanifu majengo ni sanaa ya Kiislamu ambayo inastahiki kutambuliwa. Misikiti iliyojengwa na Waislamu ambayo ilinakishiwa⁴⁴ kwa mihrab na minara ilifuata aina ya muonekano wa msikiti wa Mtume Muhammad (S.A.W) wa Madina.

SURA YA KUMI NA NNE



Mchango wa Dola ya Ottoman



Katika miaka ya baadaye, Waturuki wa Ottoman walikamilisha ustaarabu wa Kiislamu kwa kuacha athari kubwa katika sanaa na usanifu majengo. Maendeleo ya dola ya Kituruki yaliambatana na mvuvumko wa Ulaya. Waislamu walibuni aina mbalimbali za usanifu wa majengo. Waislamu wa Ottoman walibuni aina mpya ya ujenzi wa minara. Ujumuishaji wa Mihrab na sehemu ya chumba pembezoni mwake ilikuwa ni teknolojia mpya. Katika ardhi yao, Asia ya Kati, Waturuki waliishi katika mahema ambayo baadaye ilileleta athari katika sanaa na usanifu majengo katika miji waliyoishi Waturuki. Lugha yao ilikuwa ni Kituruki lakini walijifundisha fasihi na utamaduni wa Kiarabu na Kiajemi kupitia lugha ya Kiarabu na Kiajemi.

Dola ya Ottoman ilitoa kipaumbele katika ujenzi wa Misikiti kwani misikiti iliendelea kuwa ni vituo muhimu kwa dola ya Ottoman na jamii za Waislamu kwa ujumla. Kutwaliwa kwa mji wa Constantinopo mnamo mwaka 1453 ukawa mwanzo wa sanaa ya Kirumi kuwafikia Waturuki. Mafanikio haya ya kuingia sanaa ya Warumi kwa Waturuki yamepatikana kupitia utawala wa Sultan Mehmet wa pili na Sultan Sulayman. Pamoja na kuwepo kwa majengo mbalimbali ya kidini na kidunia, ikiwemo Kanisa la Hagia Sophia, ambalo Ottoman ilitwaa kutoka kwa Warumi. Baada ya Ottoman kushinda Vita dhidi ya Warumi, Kanisa hili liligeuzwa na kuwa Msikiti mkubwa na hatimaye kuwa

chimbuko la sanaa ya Ottoman. Kufikia karne ya 19 dola ya Ottoman ilikuwa tayari imefika katika mabara matatu duniani waliojitolea katika kuhimiza biashara huria na pia kuchangia kwa kiwango kikubwa kukua kwa ubepari huko Ulaya. Wasanifu ramani na waandisho wa dola ya Ottoman walitumia wasanifu ramani wa kipindi hicho cha mwamko wa maendeleo Ulaya kama vile sanaa ya kale na jigrafia ya Ptoleny⁴⁵.

Dola ya Ottoman ilikuwa ni dola ya Kiislamu ambayo ilifuatia dola za awali za ukanda wa Mediterania za Kirumi na Kiyunani, kwa hiyo Ottoman walijihesabu kama ni warithi wa utamaduni wa Kirumi na wa Kiislamu. Kama ilivyokuwa kipindi cha Ukhalifa wa Abbasiyah, dola ya Ottoman ya kiraia ilikuwa ni dola kwa ajili ya watu wote na ilichanganya tamaduni nyingi. Mfumo wa Millet uliigawa dola hii katika jamii ndogo zenye kujitawala kwa kufuata misingi ya imani zao. Uvumilivu wa kidini wa Ottoman⁴⁶ unadhihiri katika sanaa ya ujenzi. Ufungamano wao na Uislamu ulikuwepo muda wote na walidhihirisha mapenzi makubwa katika sanaa ya ujenzi ambayo iliacha athari kubwa.

Ottoman walirithi mchanganyiko wa muundo wa siasa kutoka makundi mbali mbali na kutoka katika Uislamu. Sultan, alikuwa anatokana na kiongozi muadilifu, utaratibu huu ni matokeo ya mchanganyiko wa mila na desturi za Waturuki, Waajemi na historia ya Uislamu. Sultan alikuwa na jukumu la kuwalinda watu wake dhidi ya unyonyaji wa Serikali, kama vile kutoza viwango vikubwa vya kodi, rushwa, n.k. Utaratibu huu na uvumilivu wa Ottoman ulikuwa ni kivutio kwa wageni kama vile Wayahudi waliotoka Hispania na kuishi Istanbul⁴⁷. Mwingiliano wa tamaduni ulisababisha Ottoman kuathiri na kuathiriwa na mwamko wa Ulaya kupitia kubadilishana elimu na sanaa.

SURA YA KUMI NA TANO



Mwamko Wa Maendeleo Ulaya



Watu wa Ulaya, ambao wanataka kuutokomeza Uislamu na Waislamu ndio walionufaika sana na ustaarabu wa Kiislamu, hasa katika fani za sayansi na tiba. Hata Wamongolia, ambao walijitahidi kuutokomeza Uislamu, lakini hatimaye waliukubali na kueneza ustaarabu wa Kiislamu kwa karne nyingi baadaye. Wao hasa ndio waliounda dola ya Kiislamu ya Mughal ya India, dola ambayo pamoja na dola za Safavid ya Iran na Ottoman ya Uturuki, zilifanya ustaarabu wa Kiislamu uendelee kuwepo hadi pale ukoloni wa Ulaya ulipoibuka.

Jamii ya Waislamu imeleta mageuzi na athari kubwa kwa jamii za Ulaya katika sayansi, tiba, falsafa, na fasihi. Katika taaluma ya tiba, Ulaya ilitengelea zaidi dawa za Waislamu. Elimu ya tiba ya Ulaya kwa karne nyingi ilikuwa ni mwendelezo wa elimu ya tiba ya Kiislamu. Ulimwengu wa Magharibi uliendelea kujifunza elimu ya tiba kutoka kwa Waislamu, pamoja na ukweli kwamba wameendelea kukanusha kuwa ujuzi wao wa tiba hautokani na Waislamu. Elimu ya tiba ya Kiislamu ilikuwa na ithibati hata katika nchi zinazozungumza Kiingereza kupitia maelezo ya Chancer na Shakespear.

Elimu ya Kiislamu ilifika Ulaya kupitia vituo mbalimbali vya taaluma vilivyokuwepo Hispania na Italia. Ushahidi au vyanzo vingine vinathibitisha kuwa Ulaya walipata falsafa ya Kigiriki kupitia ustaarabu wa Kislamu. Maelezo ya wanachuoni wa Kiislamu yalikuwa ni mhimili

muhimu kwa maendeleo ya Ulaya, aidha fikra za Waislamu zilijengwa na muungano wa falsafa na tiba. Mpaka ilipofikia Ulaya kuamka na kuwa mpya, lugha ya Kiarabu ilikuwa ndio lugha iliyotafsiriwa zaidi kuliko lugha yoyote duniani. Sehemu kubwa ya elimu ya Waislamu iliingia Ulaya kupitia Hispania iliyokuwa chini ya Waislamu, ambayo kwa karne nyingi ilikuwa ni kama nchi ya Mashariki ya kati walikotoka Waislamu. Hata wale wasiokuwa Waislamu walitumia majina ya Kiislamu, walivaa mavazi ya Waislamu, na walitumia lugha ya Kiarabu kwa mawasiliano. Wanafunzi Waislamu, Wayahudi na Wakristo walisafiri kwenda kusoma katika vyuo vikuu vya Waislamu vilivyokuwepo Hispania.

Mnamo karne ya 12, miaka 500 baada ya Uislamu, harakati za kutafsiri kazi zilizokuwa katika lugha ya Kiarabu kwenda kwenye Kilatini zilianza na Vitabu maarufu hasa katika sayansi, tiba na falsafa. Hata hivyo, bado Ulaya ya Wakristo haitaki kutambua elimu ya Waislamu na badala yake inadai kuwa chimbuko la elimu ya Ulaya ni Wagiriki. Mwanafalsafa Al-Farabi aliwasaidia watu wa Ulaya kwa kiu yao ya elimu, Waislamu, Wayahudi na Wakristo walisoma Vitabu vyake na kufahamu ugumu wa falsafa⁴⁸. Al-Farabi aliathiri mawazo ya watu wa Ulaya kama ilivyokuwa athari yake kwa wanachuoni wa Kikristo, Albertus na Thomas Aquinas na Wakristo kwa ujumla. Kazi zake zilijengwa katika msingi wa Quran na zilitumiwa katika kuelewa mawazo ya Aristotle, falsafa ya Kiislamu na ile ya Kikristo.⁴⁹

Uislamu vile vile uliacha athari kubwa katika fasihi kwa ulimwengu wa Magharibi. Wakati wa Zama za Kati na mvuvumko wa Ulaya, fasihi ya Kiarabu ilikuwa na athari kubwa kwa Ukristo. Vile vile miaka elfu moja ya mwanzoni, Uislamu ulikuwa wazi kwa watu wa Ulaya kupitia fasihi ya Kiarabu. Upotoshwaji unaofanywa na watu wa Magharibi dhidi ya Uislamu ulianzia na Vita vya msalaba na kuendelea baadaye. Baada ya kushindwa kupitia Vita vya Msalaba, Wakristo walijaribu kushirikiana na Wamongoli katika kuangamiza Uislamu. Ilhali ya kuwa watu wote wakiwemo wa Ulaya, wamenufaika na mafanikio yaliyopatikana kupitia ustaarabu wa Kiislamu. Kwa sababu hizi, tafsiri kutoka lugha ya Kiarabu kwenda lugha za Ulaya, pamoja na elimu na mafunzo makubwa ambayo ulimwengu wa Magharibi umeyapata kutoka kwa Waislamu, kama ni nyongeza au njia ya maarifa ya Kigiriki na sayansi ya Mashariki, ulikuwa ni mchango mkubwa kwa mwamko wa Ulaya na kwa maendeleo ya dunia ya sasa.

KIAMBATISHO



Nukuu Za Marejeo



- 1 J.M. Roberts, *The Penguin History of the World* (Harmondsworth, Middx, UK: Penguin Books, 1980), p.378.
- 2 *Ibid.*, p.62.
- 3 Franz Rosenthal, *Knowledge Triumphant* (Leiden, The Netherlands: E.J. Brill, 1970), p.70.
- 4 Qur'an 3:13, 2:118, 2:269, 31:20.
- 5 Roberts, *Penguin History of the World*, p.394.
- 6 Qur'an 38:71-72.
- 7 Qur'an 2:241.
- 8 Qur'an 2:233.
- 9 Marshall G.S. Hodgson, *The Venture*, 3 vols. (Chicago, IL, & London, 1974), vol.1, p.182.
- 10 Paul Johnson, *Civilizations of the Holy Land* (New York: Atheneum, 1979), pp.169-170.
- 11 Johnson, *Civilizations*, p.170. Also Abba Eban, *Heritage: Civilization and the Jews* (New York: Summit Books, 1984), p.127.
- 12 Philip Khuri Hitti, *History of the Arabs: From the Earliest Times to the Present*, 9th edn. (London: Macmillan; & New York: St. Martin's Press, 1968), pp.619-620.

- 13 Philip K. Hitti, *Capital Cities of Islam* (Minneapolis, MN: University of Minnesota Press, 1973), pp.510–512.
- 14 Albert Hourani, *A History of the Arab Peoples* (Cambridge, MA: Belknap Press of Harvard University Press, 1991), pp.46–47.
- 15 Bernard Lewis, *Islam and the West* (New York, and Oxford, UK: Oxford University Press, 1993), p.12.
- 16 Richard Bulliet, *Conversion to Islam in the Medieval Period* (Cambridge, MA; and London: Harvard University Press, 1979), pp.33, 34, 37, 44, 82, 97, 109 & 124.
- 17 Philip Curtin, *Cross-Cultural Trade in World History* (Cambridge, UK: Cambridge University Press, 1984), p.107.
- 18 Hitti, *History*, p.299.
- 19 Hitti, *History*, p.609.
- 20 Sayyid Fayyez Mahmud, *A Short History of Islam* (Karachi, Pakistan: Oxford University Press, 1960), p.209.
- 21 Qur'an 106:2.
- 22 *The New York Times*, March 16, 1993.
- 23 Andrew M. Watson, *Agricultural Innovation in the Early Islamic World* (Cambridge, UK: Cambridge University Press, 1983), p.2.
- 24 Janet L. Abu-Lughod, *Before European Hegemony: The World System AD 1250–1350* (New York, & Oxford, UK: Oxford University Press, 1989), p.43.
- Also, Andrew M. Watson, *Agricultural Innovation in the Early Islamic World* (Cambridge, UK: Cambridge University Press, 1983), p.22.
- 25 A.M.A. Shustery, *Outlines of Islamic Culture* (Lahore, Pakistan: Sh. Muhammd Ashraf, 1976), p.325.

- 26 Arnold Toynbee, *A Study of History* (London: Oxford University Press, 1961), vol.10, pp.64–86, vol.9, pp.175–182.
- 27 Qur'an 21:30, 24:45, 25:53-54, 34:9, 41:11.
- 28 Qur'an 25:2, 54:49 and other verses.
- 29 Colin A. Ronan, *Science: Its History and Development Among the World's Cultures* (New York: Facts on File Publications, 1982), p.203.
- 30 J. Casulleras and J. Samsó (eds.), *From Baghdad to Barcelona: Studies in the Islamic Exact Sciences in Honour of Prof. Juan Vernet*, 2 vols. (Barcelona: Barcelona University, 1996), vol. 1, p.479.
- 31 Akbar S. Ahmed, *Discovering Islam: Making Sense of Muslim History and Society* (London & New York: Routledge, 1988), pp.238–346.
- 32 George Sarton, *Introduction to the History of Science*, 3 vols. Vol.1, *From Homer to Omar Khayyam* (Baltimore, MD: Williams & Wilkins for the Carnegie Institute of Washington, 1927; repr. 1962), p.666.
- 33 Edward G. Browne, *Arabian Medicine* (Lahore, Pakistan: Hijra International Publishers, 1990), p.48.
- 34 Ahmed, *Discovering Islam*, p.221.
- 35 Reynold A. Nicholson, *A Literary History of the Arabs* (Cambridge, UK: Cambridge University Press, 1966), p.323.
- 36 Bernard Lewis, *Islam and the West* (New York, and Oxford, UK: Oxford University Press, 1993), pp.120–121.
- 37 Salma Khadra Jayyusi (ed.), *The Legacy of Muslim Spain* (Leiden, The Netherlands; New York; Cologne: E.J. Brill, 1992), pp.387–396.
- 38 H.T. Norris "Fables and Legends," in Julia Ashtiany, T.

Johnstone, J. Latham, R. Serjeant, and G. Rex Smith (eds.), *The Cambridge History of Arabic*

Literature: 'Abbasid Belles-Lettres (Cambridge, UK: Cambridge University Press, 1990), pp.137–138.

39 Reynold A. Nicholson, *A Literary History of the Arabs* (Cambridge, UK: Cambridge University Press, 1966), pp.429–430.

40 Manoochehr Aryanpur, *A History of Persian Literature* (Tehran: Kayhan Press, 1973), pp.70, 72, 73.

41 Qur'an 7:31–32, 16:8, 16:13, 50:7.

42 'Handasah al-βaw~' or 'the art of sound'.

43 Giovanni Curatola, *The Simon and Schuster Book of Oriental Carpets*, trans. Simon Pleasance (New York: Simon and Schuster, 1981), pp.28–30.

44 *Ibid.*, p.28.

45 Halil Inalcik and Cemal Kafadar, eds., *Suleyman the Second and His Time* (Istanbul: Isis Press, 1993), p.348.

46 Avigdor Levy, *Jews, Turks, Ottomans: A Shared History, Fifteenth through the Twentieth Century* (Syracuse University Press, 2003).

47 *Ibid.*

48 Muhsin Mahdi, 'Islamic Philosophy', in *The New Encyclopaedia Britannica*, Macropedia, (Chicago, IL: Encyclopaedia Britannica Inc., 1987), vol.22, pp.24–25.

49 Eugene A. Myers, *Arabic Thought and the Western World* (New York: Frederick Ungar Publishing, 1964), p.30.

KUHUSU WAANDISHI

AHMED ESSA, Twamuomba Allah amrehemu, alifariki dunia tarehe 15, Juni 2008 na Dkt. Othman Ali akasaidia kumalizia andiko la Mwisho la kitabu hiki. Dkt. Essa alikuwa Profesa katika Chuo Kikuu cha Nevada, Reno, tangu 1967 hadi 1991, akifundisha fasihi za tamaduni anuai na uandishi wa kubuni. Alikuwa msomi mashuhuri aliyebobea kwenye fasihi ya Afrika na Mashariki ya Kati. Alizaliwa India na kuishi maisha yake ya mwanzo katika miji ya Pietermaritzburg and Durban nchini Afrika Kusini. Makuzi yake katika jamii hiyo iliyokuwa na ubaguzi wa rangi yamempa uzoefu mwingi na ilhamu kwenye fani ya Uandishi wa kubuni. Dkt. Essa alikuwa pia mwasisi wa Taasisi ya Northern Nevada Muslim Society aliyeiongoza jumuiya hiyo katika uchanga na uchache wa wanachama hadi kufikia kuwa na maelfu ya wanachama hivi leo. Mnamo mwaka 2003 alitunukiwa tuzo ya World Citizen kutoka Kituo cha Kimataifa cha Nevada Kaskazini kwa kuiunganisha Nevada yenye tamaduni anuai, na watu wengine, kitaifa na kimataifa.

OTHMAN ALI ni Profesa Mkanada aliyebobea katika tafiti za Mashariki ya Kati. Ameandika kwa kina maudhui nyingi kuhusu Historia ya Mashariki ya Kati na Siasa. Amepata Shahada ya Uzamivu katika Chuo Kikuu cha Toronto na Shahada ya Uzamili katika Uhusiano wa Kimataifa kutoka Chuo Kikuu cha Guelph-Canada. Alikuwa Profesa Mshiriki katika Kitivo cha Historia na Ustaarabu, Chuo Kikuu cha Ryerson, Toronto, mwaka 1994-98. Hivi sasa ni Mhadhiri katika Kitengo cha Historia Chuo Kikuu cha Salahaddin, Erbil, Iraq. Aidha, Dkt Ali ni Rais wa Kituo cha Utafiti cha Wakurdi wa Kituruki mkoa wa Erbil-Kurdistan region of Iraq, na hamu yake hasa ni kuzama kwenye Historia na Siasa za Wakurdi.

Hiki ni kitabu kilichotoka kwa ukamilifu mwaka 2010 na kutoleshwa kwa mara ya pili mwaka 2011. Kitabu hiki kimetafiti maandiko ya wasomi wa Magharibi ili kubainisha kuwa bila ya kuwepo mchango mkubwa wa kitaaluma kutoka Ulimwengu wa Kiislamu, hakika pasingelikuwepo Mwamko wa Maendeleo uliojiri Ulaya.

Kwa takribani miaka elfu, Uislamu ulikuwa ndio ustaraabu unaoongoza duniani, ukivuka mipaka ya kijiografia na kushamiri, bila ya ubishi, kuliko ustaarabu wowote ule uliokuwepo. Uislamu uliondoa ubaguzi na utengano wa kijamii baina ya watu wa matabaka, kabila na utafa, na ukaweka wazi kuwa watu wote wanastahiki kufaidi neema za dunia maadam hawakiuki taratibu na maadili. Uislamu ndio uliozinusuru taaluma ambazo vinginevyo ama zingelipotea kwa karne nyingi au moja kwa moja.

AHMED ESSA NA OTHMAN ALI



IIIT — Mfululizo wa Vitabu kwa Muhtasari